

Kulikuwepo na bwawa lenye kingo zilizopakana na mawanda ya nyasi nyororo. Halikuwa bwawa la kawaida, lilikuwa la kipekee. Upekee gani utajiuliza. Lilikuwa na maua ya kila aina, yenye rangi nyingi kuliko unavyoweza kufikiri. Bwawa lenyewe lilikuwa na maji ya zambarau. Watu wote walikuwa wakikanya, “Yeyote atakayeyagusa au kunywa maji ya bwawa hili, atageuka kuwa chura.”







Na wala si chura wa kawaida, bali chura mwenye uwezo wa ajabu. Kama vile uwezo wa kutoa hewa ya moto wanapopumua, nguvu za kuinua vitu vizito kupindukia, kuruka juu umbali mrefu mara kumi zaidi ya binadamu wa kawaida, uwezo wa kutoa ulimi nje kwa umbali wa zaidi ya meta moja na masaibu mengine mengi.



Vyura wadogo walikuwa na uwezo wa kipekee pia. Uwezo ule ule ambao wangalikuwa nao binadamu kama wangegeuka kuwa vyura. Lakini alikuwepo chura mmoja ambaye daima alijitenga na wenzake. Jina lake ni Zakia. Alijitenga kwa sababu ya uwezo wake wa kuishi nchi kavu na majini. Alionewa na wenzake kwa sababu hiyo. Walimwona kuwa ni legelege, asiye na msisimko.


“Toka hapa, sisi tunacheza na watoto poa tu, sio watu kama wewe,” walisema.


Walikuwa wanamsukuma na kumwita ‘pumbavu’ na ‘taahira’.

Zakia alikuwa na huzuni siku zote. Alikuwa anajifungia chumbani kwake na kujilaza kitandani akiwa analia huku ameufunika uso wake kwa viganja vyake.

Zakia hakuwa na kaka wala dada. Kwa hiyo aliwaambia wazazi wake kila kitu kilichomsumbua. Mama yake hakuchoka kumwambia, “Usihuzunike Zakia, wao ndio wanajinyima faida ya kuwa na rafiki mzuri kama wewe.”

“Hivi mimi nina kasoro gani? Kwa nini wananifanyia hivi lakini?” Zakia alijiuliza mara kwa mara.





Bwawa liliendelea kuwa zuri na la kupendeza. Binadamu nao waliamini kuwa bwawa lile na viumbe waliomo ni hatari kwao. Sio tu kwa sababu maji yake yangewageuza kuwa vyura lakini pia kwa sababu ya uwezo waliokuwa nao vyura wale. Kwa muda mrefu binadamu walijaribu kuliharibu bwawa lile. Lakini hawakufanikiwa. Vyura walijibu mapigo.




Lakini kuna kitu kingeweza kuharibu maajabu ya bwawa hilo. Mchanga wa baharini. Kama binadamu wangaligundua siri hii, viumbe wa bwawani wangeangamia. Sababu ni kuwa, kama mchanga wa bahari ungetawanywa kulizunguka bwawa, vyura wangegeuka kuwa sanamu, maua yangekufa, na maji yangegeuka kuwa ya kijivu.

Siku moja asubuhi, Zakia aliamshwa na sauti kubwa za vyura wenzake waliokuwa wakilia. “Kumetokea nini?” Zakia alijiuliza kwa hofu. Haraka alikimbia nje kuangalia kuna nini. Ndipo alipojikuta akishuhudia tukio la kuogofya kupita ufahamu. “Oh! Mungu wangu! Hapana.” alipiga yowe. Zakia hakuamini macho yake. Maji ya bwawa yalikuwa yamebadilika kuwa ya kijivu. Vyura walikuwa wameganda kama sanamu; na maua yalikuwa yamekufa.




“Hii inatokana na jambo moja tu. Binadamu watakuwa wamegundua jinsi ya kuliangamiza bwawa. Sasa mimi ndiye chura pekee aliyebakia.” alijiambia akiwa nje ya nyumba yao, akilikodolea macho bwawa. Alianza kulia. Machozi yalitiririka kwenye mashavu yake kama maporomoko ya maji. “Kwa nini mimi? Kwa nini nimebaki mimi tu peke yangu. Kwa nini sijawa sanamu kama wenzangu?” alijiuliza. Kadri aliyozidi kujiuliza maswali yale, ndivyo alivyozidi kuwa na hasira. Alianza kuyapiga ngumi yale maji akiwa anawaza jinsi yalivyokuwa na rangi nzuri.




Halafu, yale maji yalibadilika ghafla yakawa ya zambarau tena. Unaweza kubashiri ni kwa jinsi gani Zakia alifurahi na kushituka. “Ndio, ndio, ndio, oh, Mungu wangu!” alipiga kelele na kurukaruka kwa furaha. “Imekuwaje jambo hili kutokea?” alijiuliza.

“Nitakuwa nimefanya nini hadi maji yakageuka kuwa ya zambarau tena?”






Alivyokuwa anajiuliza maswali, alishika maua yaliyokuwa karibu na bwawa. “Nakumbuka jinsi maua haya yalivyokuwa mazuri.” Ndipo maua yale aliyokuwa anayashika yalipozinduka ghafla na kunawiri. Zakia alipata mshituko mkubwa kuliko ule wa kwanza. Aliota matende. Aligundua kuwa anao uwezo wa kurudisha vitu vilivyoharibika kwenye ubora wake wa awali kwa kuvigusa tu na kufikiria jinsi vilivyokuwa kabla ya kuharibika. Alifurahi sana. Ndipo alipoanza kuyafufua maua yote yaliyokuwa yamekufa. Kisha alikaa ukingoni mwa bwawa akiwaza, “Kama ninaweza kuyafufua maua, je nitaweza kuwarudisha vyura wezangu? Kuna njia moja tu ya kupata uhakika. Lazima nijaribu.”



Mara baada ya kufikiria hivyo alimkimbilia mama yake. Kabla hajamfufua alimkodolea macho kwa huzuni, machozi yakimlengalega. Kisha alijaribu kumfufua mama yake.



“Nakumbuka jinsi mama yangu alivyokuwa. Alikuwa anapumua, yuko hai. Halafu mama yake akafumbua macho. “Mama! Mama! Unanisikia?” Zakia aliuliza. Mama Zakia aliuliza, “Kwani kumetokea nini?”

Zakia alimsimulia mama yake kila kitu kilichotokea pamoja na uwezo wake mpya aliougundua.

Halafu aliendelea kuwafufua vyura wenzake waliosalia.



Hatimaye, Zakia akiwa na umri wa miaka 15 alichaguliwa kuwa kiongozi wa jumuiya yao ya vyura. Si kwa sababu tu ya uwezo wake bali ni kwa sababu ya ujasiri wake na uwezo wa kufikiri kwa haraka. Basi aliendelea kuiongoza jumuiya yake na bwawa limekuwa hai milele.

